**MKATABA WA KUPANGISHA GODOWN LILILOPO KIWANJA NAMBA 23, KITALU "…………" KISESA VILLAGE WILAYA YA ILEMELA MKOA WA MWANZA**

**SHERIA YA MKATABA**

**( SURA YA 345)**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe ……28……Mwezi……July……mwaka **2024**

**KATI YA**

**MUNIREMA CONSTRUCTION (LTD) wa S.L.P 10094 ,DAR ES SALAAM-TANZANIA** ambao ni kampuni iliyosajiriwa kwa mujibu wa sheria za hapa nchini Tanzania (ambao katika Mkataba huu watajulikana kama "**WAPANGISHAJI**") kwa upande mmoja.

**NA**

**WIMATEC INVESTMENT LTD** wa **S.L.P 3652, DAR ES SALAAM-TANZANIA** ambao ni kampuni iliyosajiriwa kwa mujibu wa sheria za hapa nchini Tanzania (ambao katika Mkataba huu watajulikana kama "**WAPANGAJI**") kwa upande mwingine.

**KWA KUWA** MPANGISHAJI ni mmiliki halali wa Godown lililopo katika Kiwanja Na. **"23"** Kitalu **"……….", KIESESA VILLAGE** wilaya ya **ILEMELA** Mkoa wa **MWANZA.**

**NA KWA KUWA MPANGISHAJI** amekubali kumpangisha **MPANGAJI** katika Godown hilo tajwa hapo juu kwa matumizi ya biashara zake na kuwa mkataba huu utaanza tarehe **01/08/2024** hadi tarehe **01/08/2026.**

**BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

1. **MPANGISHAJI** anampangisha mpangaji **Godown hilo** lililopo katika kiwanja tajwa hapo juu kwa kodi ya T.Shs **MILIONI SITA TU (6,000,000/=)** kwa mwaka.

2. Kwamba kipindi cha Mkataba huu kitaanza rasmi tarehe **01/08/2024** na utafika kikomo tarehe **01/08/2026.**

3. Kwamba, kwa kusaini mkataba huu **MPANGISHAJI** anakiri kuwa amepokea kiasi cha **T.Shs. MILIONI SITA TU (6,000,000/=)** taslimu kama malipo ya pango kwa muda wa mwaka mmoja tu kuanzia tarehe **01/08/2024** mpaka tarehe **01/08/2025.**

4. **Kwamba, MPANGISHAJI** anakiri kuwa hakutakuwa na ongezeko la kodi kwa mpangaji kwa kipindi cha miaka mitatu ya upangishaji.

**MPANGAJI ANAKUBALIANA NA MWENYE NYUMBA KAMA IFUATAVYO:**

a. Kwamba, mpangaji atalipa kodi kwa wakati kama ilivyokubaliwa katika mkataba huu na kwamba kama mpangaji akishindwa kulipa kodi kwa wakati basi mpangishaji atamwondoa katika Godown lake.

b. Kwamba, itakuwa ni wajibu wa Mpangaji kulipa bili zote za maji, umeme na kutunza Gowdown hilo pamoja na mazingira yake katika hali ya usafi kama alivyokuta.



CamScanner

c. **KWAMBA, MPANGAJI** atawajibika kuhakikisha mazingira ya nyumba Godown hilo yanakuwa katika hali ya usafi na salama kwa matumizi ya binadamu kama alivyokuta.

d. **KWAMBA, MPANGAJI** atawajibika kutunza Godown hilo pamoja mazingira yake katika hali nzuri kama alivyovikuta na kwamba mpangaji atawajibika kwa kila uharibifu atakaousababisha kwenye Godown hilo kwa uzembe wake mwenyewe.

e. **KWAMBA,** kama mpangaji akitaka kufanya marekebisho katika Godown hilo anapaswa kumtaarifu mpangishaji kabla ya kufanya matengenezo na Kwamba, **MPANGAJI** atamruhusu mpangishaji kuingia na kukagua matengenezo baada ya mpangaji kutoa taarifa ya kufanya hivyo.

f. Kwamba Mpangaji kwa namna yoyote ile hatapangisha Godown hilo kwa mtu mwingine bila ridhaa ya mpangishaji.

g. Kwamba mpangaji atamkabidhi mpangishaji, Godown hilo likiwa katika hali nzuri kama alivyoikuta mara baada ya kipindi cha mkataba kumalizika isipokuwa tu kama mkataba huu utakuwa umeongezwa muda kwa kipindi kingine.

**MWENYE NYUMBA ANAKUBALIANA NA MPANGAJI KAMA IFUATAVYO:**

a. Kwamba, kipindi cha Mkataba huu kitaanzia tarehe **01/08/2024** hadi tarehe **01/08/2026.**
b. Kwamba kama mpangaji atatimiza masharti ya mkataba huu atatumia Godown hilo bila kubughudhiwa katika kipindi chote cha mkataba huu.

c. Kwamba, godown hilo halijapangishwa kwa mtu yeyote isipokuwa mpangaji aliyetajwa katika mkataba huu.

d. Kwamba, iwapo kutatokea hali yoyote ile ya kusitisha Mkataba huu Kwa upande wa Mpangishaji basi atarudisha kodi ya pango kwa miezi iliyosalia na kwa upande mwingine kama mpangaji akitaka kusitisha mkataba hatarudishiwa kodi iliyosalia.

e. Kwamba, Mkataba, huu unaweza kuongezwa muda kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja na kipengele chochote kinaweza kubadilishwa kwa makubaliano ya maandishi kati ya pande zote mbili.

f. Kwamba, Upande wowote unaweza kusitisha mkataba kwa kutoa notisi ya Mwezi mmoja yaani siku thelathini tu (30).

g. Endapo utatokea mgogoro wowote ule juu ya makubaliano haya, basi njia ya usuluhishi na majadiliano itatumika kati ya mpangishaji na mpangaji.

Steven Emmanuel Makwega
Box 1214 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths



CamScanner

h. Mkataba huu utatawaliwa na sheria za nchi na sheria za mkataba.

**KWA KUTHIBITISHA MAKUBALIANO** haya, pande zote zimeweka saini zao kwa namna na katika tarehe inayoonyeshwa hapa chini.

**IMESAINIWA HAPA MWANZA**
na **MUNIREMA CONSTRUCTION (LTD)**
ambaye ametambulishwa kwagu na
.......................................................
Ambaye ninamfahamu binafsi
Leo tarehe....28.....mwezi.....07.......**2024**

.................................
**MPANGISHAJI**

**MBELE YA**
**JINA:** ...ERNEST KAMIL MREMA...
**SAHIHI:** .......................................
**ANWANI:** ..P.O. BOX 10094, DAR ES SALAAM.
**WADHIFA:** ..MKURUGENZI.................

**MBELE YANGU:**
**JINA: STEVEN E. MAKWEGA**
**SAHIHI:** .......................................
**ANWANI: S.L.P 1214, MWANZA**
**WADHIFA: WAKILI**

Steven Emmanuel Makwega
Box 1214 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

**IMESAINIWA** hapa **MWANZA** na
**WIMATEC INVESTMENT LTD**
ambaye ametambulishwa
kwangu na.......................................................
ambaye ninamfahamu binafsi
leo tarehe ....28.....mwezi .....07.....**2024**

**MPANGAJI**

**MBELE YA**
**JINA:** ...JAPHARY EMMANUEL MUMSI
**SAHIHI:** .......................................
**ANWANI:** ..P.O. BOX 3652, DAR ES SALAAM
**WADHIFA:** .......MKURUGENZI..........

**MBELE YANGU:**
**JINA: STEVEN E. MAKWEGA**
**SAHIHI:** .......................................
**ANWANI: S.L.P 1214, MWANZA**
**WADHIFA: WAKILI**

Steven Emmanuel Makwega
Box 1214 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths



CamScanner